**TAMKO LA WADAU NA MASHIRIKA YA UTETEZI WA HAKI ZA BINADAMU JUU YA SHAMBULIZI DHIDI YA MHE. TUNDU LISSU NA VITENDO VINAVYOTIA HOFU ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU NCHINI**

**Ndugu Watanzania ,**

Wadau na mashirika ya utetezi wa haki za binadamu Tanzania tumeshtushwa sana na tunalaani shambulio na jaribio la kumuua Mhe. Tundu Lissu ambaye ni Mbunge na Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) lililofanyika siku ya tarehe 7/9/2017 akiwa mkoani Dodoma alipokwenda kuhudhuria mikutano ya Bunge. Kwa pamoja kama wadau wa haki za binadamu, tunalaani vikali shambulio hilo ambalo limehatarisha maisha, na kusababisha taharuki kubwa kwa Watanzania wote hasa familia ya Mhe.Lisu ambayo mpaka sasa iko katika majonzi makubwa.

Sisi watetezi wa haki za binadamu tumekuwa tukafatilia kwa ukaribu matukio mbalimbali ya kinyama, kikatili na yasiyokubalika yanayoendelea nchini kinyume na haki za binadamu. Matukio haya yanaota mizizi kwa kasi kwa kukosa ufumbuzi na hivyo kuongeza hofu baina ya wapenda amani, watetezi wa haki za binadamu na wananchi kwa ujumla. Utawala wa sheria, haki na uhuru wa maoni unazidi kupotea hapa Tanzania kila kukicha na wale wote wanakosoa hali hii wamekuwa katika mazingira magumu ya usalama wao.

**Ndugu Watanzania,** siku ya tarehe 26/8/2017 tulipokea taarifa za kuvamiwa na kulipuliwa na mabomu kwa ofisi ya mawakili wa IMMA hapa Dar es Salaa tukio ambalo liliambatana na kutekwa nyara kwa walinzi wa kampuni hiyo.Tukio hilo likiwa bado kwenye hatua ya upelelezi, tulisikistishwa kupata taarifa nyingine kwamba Mhe. Tundu Lisu ameshambuliwa kwa risasi mkoani Dodoma ikiwa ni sehemu ya matukio ya kinyama zaidi kuwahi kutokea nchini hasa kwa viongozi kiongozi na mtetezi kama Tundu Lisu.

**Tundu Lisu Mtetezi wa Haki wa Muda Mrefu**

**Ndugu Watanzania,** Mhe. Tindu Antipas Lisu amekuwa mwanaharakati wa muda mrefu wa utetezi wa haki za binadamu na Rasilimali za Nchi pamoja mambo mengi ambayo yanastahili

heshima kubwa katika katika ulinzi wa haki za binadamu na utawala bora kitaifa na kimataifa. Kabla ya kuwa mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2010 Mh. Lisu alifanya kazi na Shirika LEAT(Lawyers Enviromental Action Team) kwa kipindi cha miaka 10 (1998-2008) na katika miaka hiyo alishiriki kwa ujasiri na ufahamu mkubwa katika kampeni mbali mbali za kupigania utunzaji bora wa mazingira na maliasili za nchi yetu.

Aidha, alishiriki katikakampeni za kufichua jinsi ambavyo madini ya nchi yetu yalikuwa yanaporwa kupitia mikataba mibovu ya madini pamoja na sheria mbovu za madini, kodi, na mauzo. Aliwasemea bila woga wachimbaji wadogo walioporwa migodi yao na kampuni hizo zikisaidiwa na vyombo vya dola vya nchi yetu.  Kutokana na kazi yake hii ya utetezi ameshashitakiwa mara nyingi katika mahakama mbalimbali hapa nchini na kushinda mashauri hayo yaliyolenga kumzuia na kazi hiyo ya utetezi wa haki.

Na hata baada ya kuchaguliwa kuwa Mbunge  na wananchi wa Singida Mashariki kuanzia mwaka 2010 -2017 ameeendelea kuwa mtetezi imara wa utawala bora, haki sa kisiasa,  misingi ya haki za binadamu na rasilimali za taifa. Jitihada zake  pamoja na wadau wengine zimeweza kuleta matokeo makubwa ikiwemo hatua mbalimbali ambazo serikali ya awamu ya tano imezichukua ikiwa ni pamoja na kubadilisha sheria za madini na petroli pamoja na kuanza majadiliano na makampuni na makampuni ya madini. Hivyo mtu huyu badala ya kumlipa kwa risasi zaidi ya 30 ,alipaswa kukumbatiwa kama hazina kubwa katika siasa, utetezi, sheria na rasilimali madini  hapa Nchini.

**Ongezeko la Matukio ya Kutisha kwa Raia na Watetezi**

**Ndugu Watanzania,** katika kipindi cha miaka miwili iliyopita kumekuwa na matukio kadhaa ya ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na haki za binadamu yakiambatana na vitendo vya mauaji, utekwaji na manyanyaso kwa,  watetezi wa haki za binadamu,  viongozi wa kisiasa , maafisa wa polisi na wananchi.Matukio haya yameendelea kuleta hofu baina ya wananchi kuhusu hali ya usalama nchini .Baadhi ya matukio haya ni kama kamaifuatavyo;

i. Mwaka 2015, kijana George Mgoba ambaye ni mtetezi wa haki za vijana, kutoka "National Youth Service".Katika hali ya kushangaza, tarehe **16/2/2015**, Mgoba alipotea.

Baadae taarifa za kupatikana kwake zilienea, huku ikiripotiwa kuwa alikutwa ametelekezwa maeneo ya Kibaha nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam akiwa amenyolewa nywele nusu-kichwa.Baadae, kituo cha Polisi Kisutu, Dar es Salaam baadala ya kuchunguza tukio hilo, kilimshtaki yeye pamoja na watetezi wenzake watano wa haki za binadamu kwa kesi ya jinai namba 38 ya 2015, kwa kuendesha mkutano kinyume na sheria. Hadi sasa hakuna uchunguzi wala hatua yoyeote iliyochukuliwa kwa wahusika walio mteka.

ii. Tarehe **18/3/2016**, tulipata taarifa ya kwamba Bi. Salma Said ambaye ni mwandishi wa Mwananchi Communications Ltd. na mwandishi wa Kampuni ya Kimataifa ya Ujerumani (Deutsche Welle) alipotea katika hali ya kutatanishana taarifa zake kuzagaa kwenye vyombo vya habari kote Nchini. Hat hivyo alipatikana siku kadhaa baadaye.Bi Salma alieleza kwamba,alishambuliwa na watu wasiojulikana ambao walimchukua na kumpeleka kusikojulikana mara baada ya kutoka nje ya maeneo ya uwanja wa kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere.Hadi sasa toka Bi. Salma taarifa Polisi hakuna taarifa za uchunguzi zilizo tolewa kuhusu watekaji hao mpaka sasa.

iii. Tarehe 18 /11/ 2016 Ndugu Benard Focus Saanane au maarufu kama Ben Saanane aliondoka nyumbani kwake maeneo ya Tabata jijini Dar es Salaam, na tangu siku hiyo hajaonekana tena hadi leo. Taarifa za kupotea kwake zilitolewa kwa jeshi la polisi Makao makuu siku ya tarehe 05/12/2016 na kusajiliwa kwa namba TBT/RB/8150/2016 lakini hakuna taarifa za uchumguzi zilizotolewa kuhusu kupotea kwake mpaka sasa.

iv. Tarehe 08/12/2016 ziliripotiwa taarifa za kuokotwa kwa miili ya watu 7 huko Bagamoyo eneo la mto Ruvu. Kwa kuwa familia ya Beni Saanane na watanzania wengine waliopotelewa na ndugu zao zilikuwa katika taharuki ililazimika kusafiri kwenda Bagamoyo kujiridhisha kama miili iliyookotwa inahusiana taarifa hizo . Hata walipofika walikuta miili hiyo ilishazikwa na Jeshi la Polisi na hakunataarifa zozote za uchunguzi zilizotolewa mpaka sasa.

v. Tarehe 17/03/2017 taarifa zilienea kwenye vyombo vya habari kwamba Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Paul Makonda akiwa na watu wanaodhaniwa kuwa ni askari alivamia Kituo cha Televisheni cha “Clouds Media Group” wakiwa na silaha za moto na kulazimisha kipindi kurushwa .Baada ya kutokea kwa tukio hilo Waziri aliyekuwa na dhamana Ndugu Nape Nnauye alichukua hatua ya kuunda kamati ambayo ilitoa Taarifa kuhusu tukio hilo. Hata hivyo baada ya taarifa hiyo kutolewa, Rais alimfukuza kazi waziri huyo na kuwaacha Watanzania na maswali mengi kwani waliamini kwamba Waziri alitekeleza wajibu wake na alistahili pongezi na si kufukuzwa kazi.

vi. Tarehe 23/3/2017 Mh. Nape Mnauye wakati akiwa kwenye mkutano na vyombo vya habari alivamiwa na watu wasiojulikana na kutishiwa kupigwa risasi kwa bastola.Tukio hilo lilitokea hadharani na kurekodiwa mitandaoni Hata hivyo hakuna taarifa zaidi za upelelezi na hatua zilizochukuliwa kuhusu tukio hilo mpaka sasa.

vii. Tarehe 6/4/2017 Msanii maarufu Roma Mkatoliki pamoja na Rapa Moni Central Zone walitekwa na watu wasio julikana wakiwa kwenye shughuli zao Tongwe studio. Wasanii hao walipatikana siku kadhaa baadae na kukiri kutekwa na watu wasiojulika.Hata hivyo hakuna taarifa zaidi za upelelezi na hatua zilizochukuliwa kuhusu tukio hilo mpaka sasa.

viii. Tarehe 22/4/2017 kituo kilipokea taarifa za kuvamiwa kwa mkutano wa CUF uliokuwa unafanyika katika Hoteli ya Vina Mabibo na watu wasiojulikan wakiwa na silaha na kuanza kuwapiga wanachama na wandishi wa habari. Hata hivyo kwa jitihada za wananchi baadhi ya watu hao walikamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya dola. Hata hivyo hakuna taarifa zaidi za upelelezi na hatua zilizochukuliwa kuhusu tukio hilo mpaka sasa.

ix. Kuanzia mwanzo mwa mwaka 2017 vyombo vya habari vimeendelea kutoa taarifa mbalimbali za mauaji ya kinyama wilayani Kibiti yakihusisha viongozi wa kisiasa, wananchi pamoja na askari wa Jeshi la Polisi na kugharimu zaidi ya maisha ya watanzania 40 na askari polisi 20. Pamoja taarifa hizo na jitihada zilizooneshwa na

vyombo vya dola mpaka sasa taarifa kamili za uchunguzi kuhusu wahusika wa matukio hayo hazijawa wa kurizisha.

x. Tarehe 20th July 2017 Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kibondo Mh. Simoni Kanguye alitekwa na watu wasio julikana mbele ya ofisi ya Halmashauri, Mkurugenzi wa Manisapaa pamoja na wananchi. Baada ya tukio hilo taarifa zilifikishwa katika kituo cha Polisi na kusajiliwa kwa namba ,**KBO/RB/1225/2017**. Hata hivyo hakuna taarifa zaidi za upelelezi na hatua zilizochukuliwa kuhusu tukio hilo mpaka sasa.

xi. Mnamo tarehe 3 Juni 2017 mkutano wa ndani uliofanywa kwa mujibu wa sheria ulizuiwa na kusababisha kufunguliwa kwa mashtaka dhidi ya watetezi wawili wa haki za binadamu, Onesmo Olengurumwa na Baraka John Mbwambo. Mkutano huo ulikuwa wa uzinduzi wa kitabu kilichoandikwa na kijana Mtetezi wa Haki za Binadamu, Alfonce Lusako ambaye alifukuzwa kutoka masomo yake ya Chuo Kikuu. Amri ya kukamatwa ilidaiwa kuwa ilitoka kwa watu wasiojulikana ndani ya serikali.

xii. Mnamo Julai 4, 2017, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Salum Hapi, alitoa amri ya kukamatwa kwa Mbunge wa Kawe, Halima Mdee kwa madai kwamba mbunge huyo alitoa maneno yenye kuudhi dhidi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo Mbunge huyo, alikuwa akitumia haki yake ya Kikatiba ya uhuru wa kujieleza lakini akajikuta kwenye mikono ya polisi kwa muda mrefu baada ya kukataliwa dhamana ya polisi.

xiii. Mnamo Desemba 2016, Haki Madini, Shirika la Kiraia ambalo pamoja na mambo mengine, linahusika na utetezi wa haki za watu wanaofanya kazi katika sekta ya uchimbaji wa madini walikwenda wilaya ya Shinyanga kufanya utafiti juu ya haki ardhi kwa wanawake lakini walizuiliwa na Mkuu wa Wilaya ambaye aliwaomba barua ya kibali kutoka kwa Kamishna wa madini na Wizara ya Nishati na Madini.

xiv. Tarehe 19/8 2017 tulipokea taarifa kupitia vyombo vya habari kuhusu kuuwawa kwa kupigwa risasi kwa Mwanaharakati wa kuhifadhi wanyama pori Wyne Lotter akiwa nyumbani kwake masaki na watu wasiojulikana. Taarifa za tukio hilo lilitangazwa

kwenye vyombo vya habari kote nchini. Hata hivyo hakuna taarifa zaidi za upelelezi na hatua zilizochukuliwa kuhusu tukio hilo mpaka sasa.

xv. Jana usiku tarehe 8/9/2017 baada ya taarifa ya Lisu kutolewa kwenye vyombo vya habari tulipokea taarifa za kuvamiwa kwa ofisi za Chadema Morogoro Mjini na watu wasiojulikana na kumchukua kwa nguvu msaidizi wa Ofisi hiyo Ndugu Ibra ambaye mpaka hivi sasa hajulikani aliko.

xvi. Kwa ujumla tunasema na sisi kama watetezi wa haki za binadamu tumetambua kuwa hatupo huru na salama kwani baadhi yetu humu tayari wameshaanza kuona matukio yenye viashiria vibaya.

**Mapendekezo Yetu**

Wadau pamoja na jumuia ya watetezi wa haki za binadamu tunasikitishwa sana na vitendo hivi vya kinyama , kikatili , na vinavyo tishia hali ya ulinzi wa haki za binadamu nchini.Hivyo tunatoa mapendekezo yafuatayo:

1. Kwa pamoja tunamtaka waziri wa Ulinzi Mh, Mwigulu Nchemba ajiuzulu haraka iwezekenavyo kutoka katika nafasi yake ili kuonyesha uwajibikaji wake kiuongozi kwa kushindwa kusimamia vyema usalama wa raia na mali zao.

2. Serikali, kupitia Jeshi la Polisi, kuhakikisha wanafanya upelelezi wa hali ya juu wamatukio yote na kuwakamata wahusika wa unyama huu na kuwachukuliwa hatua kali za kisheria.

3. Watu wote waliotajwa au kuonekana waziwazi katika vyombo vya habari hasa waliomshambulia Mh, Nape Mnauye , walio vamia kituo cha Redio cha Clouds FM na walio vamia mkutano wa CUF maarufu kama watu wasiojulikana wakamatwe na wafikishwe mahakamani haraka iwezekanavyo kujibu tuhuma zinazowakabili.

4. Serikali ya Tanzania inapaswa kuzingatia misingi ya kimataifa ya haki za binadamu kama ilivyoainishwa katika Mikataba ya Umoja wa Mataifa ambayo Tanzania ni mwanachama. Kwa sababu hii, tunapendekeza kwamba serikali inapaswa kutia sahihina kuridhia

Mkataba wa Kimataifa wa kwa Ajili ya Ulinzi wa Watu Wote Waliotekwa na Kuwekwa Vizuini.

5. Tasnia ya sheria iachwe huru katika kufanya kazi zake na kupatiwa ulinzi kwa mujibu wa sheria.Mahakama, kama mhimili muhimu katika usimamizi wa haki, ina wajibu wa kuhakikisha kwamba maofisa wote wanaofanya kazi chini ya mhimili huo wanakuwa salama na wanalindwa kwa mujibu wa sheria katika kutekeleza majukumu yao .
6. Viongozi wa Dini wachukue hatua madhubuti kukemea matukio kama haya kwa nguvu kubwa kwani mwisho wa matukio haya ni kuvunjika kwa amani Nchini.
7. Viongozi wa siasa na Bunge wajadili kwa kina maswala ya usalama na haswa swala la utekwaji na mashambulizi ya kinyama kwa wananchi na kutoa mapendekezo yatakayoleta suluhu ya kudumu kwa usalama wa Nchi.
8. Wananchi kuwa mstari wa mbele kuripoti matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu, na uhalifu, ikiwemo mauaji mbalimbali yenye utata kwa vyombo vya dola na vituo vya kutetea haki za binadamu bila woga. Jukumu la kulinda haki za binadamu ni letu sote, sio la wanasheria, watetezi wa haki za binadamu, maafisa wa vyombo vya dola au viongozi katika ngazi mbalimbali pekee;
9. AZAKI, vyombo vya habari na umma wa watanzania kwa ujumla tunapaswa kuwa mstari wa mbele kukemea vitendo vyovyote ambavyo vinalengo la uvunjifyu wa Amani na kuzuia uhuru wa maoni nchini Tanzania.
10. Viongozi waheshimu haki za kisiasa na wanasiasa kwa kuwa mfumo wa vyama vingi upo kikatiba na kisheria.
11. Serikali na vyombo vyote vya usalama vihakikishe sisi kama watetezi tunabakia salama kwani sio wote wanaofurahia au kupendezwa na kazi tunazozifanya.

**Hitimisho**

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 14 inasema***"kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria".***

Ibara ya 8 (1) (c ) ya katiba inasema zaidi kwamba, ***"Tanzania ni Nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hivyo - Serikali itawajibika kwa wananchi"***

Kulingana na hali halisi ya usalama nchini Serikali inawajibika kikatiba kuchukua jitihada za dhati kuimarisha ulinzi wa haki hizo. Matukio ambayo yamekuwa yanatokea lazima yapewe

uzito unaostahiki kwani hali ikiendelea hivi  Tanzania itapotea hadhi iliyojijengea muda mrefu ya kuitwa “kisiwa cha amani.”Tukumbuke hakuna nchi duniani iliyoingia kwenye hali kama hizi ikabaki salama.

Imetolewa na

1. KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU
2. MTANDAO WA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU TANZANIA.
3. WOMEN IN LAW AND DEVELOPMENT IN AFRICA (WILDAF)
4. ACTIONS FOR DEMOCRACY AND LOCAL GOVERNANCE
5. AHADI FORUM TANZANIA (AFTA)
6. ASSOCIATION FOR NON GOVERNMENTAL ORGANISATION ZANZIBAR (ANGOZA)
7. ASSOCIATION OF RARE BLOOD DONOR (ARBD)
8. ASYLUM ACCESS TANZANIA (AATZ)
9. AVIWATA
10. BETHANIA EMPLOYEMENT AND SUPPORT (BEST)
11. BETTER LIFE
12. BIHARAMULO NGOS NETWORK FORUM
13. CENTRE FOR PROMOTION OF HUMAN RIGHTS
14. CESOPE
15. CORDS
16. DEFENCE OF HUMAN RIGHT / CITIZEN RIGHT (DHR/CR)
17. DUNGONET (NGO’S NETWORK FOR DODOMA)
18. FOUNDATION FOR HUMAN RIGHTS AND COMMUNITY DEVELOPMENT(FHC-RD
19. GOSPEL COMMUNICATION NETWORK OF TANZANIA
20. HAKI CATALYST
21. HAKI MADINI
22. HAKI ZA BINADAMU NA RAIA
23. HUMAN RIGHTS NATIONAL ASSOCIATION OF EDUCATORS FOR WORLD PEACE
24. INITIATIVE FOR GOOD GOVERNANCE AND TRANSPARENCE IN TANZANIA (IGT)
25. JUKWAA LA KATIBA
26. JUMAVIWACHA
27. JUMUIYA YA KUENDELEZA UFUGAJI NYUKI NA UHIFADHI MAZINGIRA (JUKUNUM)
28. JUMUIYA YA KULINDA NA KUTETEA HAKI ZA WANAWAKE NA WATOTO MKOANI (JUKUWAM)
29. KASULU LEGAL AID
30. KIGOMA AND UJIJI NON-GOVERNMENTAL ORGANISATION
31. KIGOMA WOMEN DEVELOPMENT
32. KITUO CHA WASAIDIZI WA KISHERIA CHA JAMII (KIWAKIJA)
33. LARETOK-LE-SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU NGORONGORO (PAIDECO)
34. LHRC
35. LINDI EDUCATION DEVELOPMENT ORGANISATION (LEDO)
36. LIWALE FARMERS ASSOCIATION (LIFA)
37. MAIPAC
38. MBEPAU
39. MBEYA HOPE FOR OPHARNS
40. MBEYA WOMEN
41. MEDIA ASSOCIATION FOR INDIGENOUS AND PASTORALIST COMMUNITIES

42. MIKONO YETU CENTRE FOR CREATIVITY AND INNOVATION (MIKONO YETU)
43. MISA TAN
44. MOROGORO PARALEGAL CENTRE (MPLC)
45. MTWARA PARALEGAL CENTRE
46. MUKEMBA GROUP MAENDELEO
47. MUSODEO
48. NEW HOPE NEW WINNERS FOUNDATION (NHNWF)
49. NGUVUMALI COMMUNITY DEVELOPMENT OF ENVIRONMENT
50. PAICODEO
51. PARALEGAL PRIMARY JUSTICE (PPJ)
52. PEMCO
53. PINGOS FORUM
54. RESOURCE ADVOCACY INIATIATVE (RAI)
55. ROWODO
56. RUANGWA ORGANISATION FOR POVERTY ALLAEVIATION (ROPA)
57. RURAL WOMAN DEVELOPMENT INITIATIVE (RUWODI)
58. RUVUMA PRESS CLUB
59. SAHARINGON
60. SERVICE HEALTH AND DEVELOPMENT FOR PEOPLE
61. SHIRIKA LA BINADAMU NANDANGALA
62. SIKIKA
63. TANGA PARALEGAL AID
64. TANZANIA CENTRE FOR RESERCH AND INFORMATION ON PASTORALISM (TCRIP)
65. TANZANIA HOME ECONOMIC ASSOCIATION (TAHEA) BIHARAMULO
66. TANZANIA LEGAL KNOWLEDGE AND AID CENTRE
67. TANZANIA MEDIA WOMANS ASSOCIATION (TAMWA)
68. TANZANIA NETWORK OF LEGAL PROVIDERS (TANLAP)
69. TANZANIA PARTNERSHIP DEVELOPMENT ORGANISATION
70. TANZANIA PASTORALIST COMMUNITY FORUM (TPCF)
71. TANZANIA WIDOWS ASSOCIATION
72. TANZANIA WIDOWS ASSOCIATION (TAWIA)
73. TANZANIA YOUTH POTENTIAL ASSOSIATION
74. TAS
75. TAWLA
76. TCIB
77. TGNP MTANDAO
78. THE DEVELOPMENT FOR ACCOUNTABILITY FOR TANZANIA
79. THE ORGANISATION OF JOURNALISTS AGAINST DRUG ABUSE AND CRIMES IN TANZANIA (OJADACT)
80. TNRF
81. TUPACE
82. UMOJA WA VIKUNDI VYA UZALISHAJI MALI NA UELIMISHAJI RIKA MAGU
83. UNDER THE SAME SUN (UTSS)
84. UTPC
85. UVINZA NGOS NETWORK (UNON)
86. WOMEN WAKE-UP (WOWAP)
87. WORLD YOUTH ALLIANCE
88. WOTE SAWA YOUTH DOMESTIC WORKERS
89. YOUTH AGAINST AIDS POVERTY

90. YOUTH TO YOUTH
91. ZAFELA
92. ZANZIBAR AIDS ASSOCIATION AND SUPPORT FOR OPHARNS (ZASO)
93. ZANZIBAR ASSICIATION FOR CHILDREN ADVANCEMENT (ZAC)
94. ZANZIBAR FIGHTING AGAINST YOUTH CHALLENGES ORGANIZATION (ZAFAYCO)
95. ZANZIBAR LEGAL SERVICES CENTRE (ZLSC)
96. COMMUNITY FOR EDUCATORS AND LEGAL ASSISTANCE
97. HAKI MADINI
98. ANGOZA
99. ZAFELA
100. ZLS
101. TAWIA
102. Media Council of Tanzania